**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Mkuu wa Shule 0763518938**
**Mkuu wa Shule.0622730576**
**Matron 0762071459 /Patron0655605291**

**SHULE YA SEKONDARI MTWANGO Makamu**
**S.L.P 370,**
**NJOMBE.**

**imail:mtwangosekondari@njombedc.go.tz.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………......................**

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA …………………**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya sekondari MTWANGO mwaka …………….. .Hongera sana. Shule ni ya bweni kwa wasichana na wavulana.

Shule ya Sekondari Mtwango ipo barabarakuu ya makambako - Njombe au Njombe -makambako umbali 25 KM kutoka makambako hadi mtwango stendi nauliTsh 3000 na Njombe stendi hadi Mtwango stendi km 34 nauli yakeTsh 3000 kutoka barabara kuu mpaka shuleni km 2 Usafiri wa pikipiki Tsh 3000 kutoka stendi ya mabasi mtwango hadi shule ilipo.

Muhula wa Masomo utaanza tarehe **06/07/2025.** Kuripoti shule ni kadri ya Tangazo la serikali.

2.**KAULI MBIU YA SHULE ’’ EDUCATION HAS NO END’’**

Kauli hiyo ndiyo itakuwa dira ya mwanafunzi wakati wote atakopokuwa hapa shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili.Mwanafunzi anatakiwa kuitafakari kauli mbiu hiyo kwa vitendo,Nimatumaini yetu kuwa mwanafunzi atatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yake na taifa kwa ujumla.Hivyo basi,atatakiwa kuwa na tabia njema na ahudhurie masomo na kujifunza kwa bidii.

Uongozi wa shule unahimiza ufaulu katika Taaluma usipungue alama 65% bila hivyo ni utovu wa nidhamu.Tahasusi zinazotolewa hapa shuleni ni HGL,HGK,HKL, HGFa, HGLi na CBG

Timiza wajibu wako.
Elimu haina mwisho.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MTWANGO
S L P 370, NJOMBE

**VERONICA T.MFUGALE**
**MKUU WA SHULE**

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

**2.2 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | AinayaMchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango hiyo ilipwe kupitia akaunti namba 0150673189300 CRDB, jina la akaunti ni MTWANGO SECONDARY SCHOOL .Tafadhari andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye ”pay in slip” .Pindi afikapo shuleni aiwasilishe kwa mhasibu wa shule.**

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni**

i. Madaftari (counter book quire 3 au 4 )**10**

**ii.** **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka;(kila muhula toa ream 01)isipokuwa tahasusi ya CBG waje na **Ream (A3) moja (01)**

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology

v. Scientific Calculator (silent non-programmable with function fx -99IMS) kwa Tahasusi za CBG, HGL na HGK

vi. Laboratory coat –rangi nyeupe kwa wanafunzi watahasusi ya CBG tu.

vii. Godoro 01 INCH 2 ½ ,mto, Mashuka na foronya pair 2 rangi ya **light-blue** kwa wavulana na rangi ya **pinki** kwa wasichana, blanket 01 zito hali ya hewa ni baridi ,

viii. Torch ya solar 01 kwa matumizi yake binafsi nyakati za usiku (ingawa umeme upo)

ix. Nguo za ndani za kutosha;

x. Tranka lenye kufuri kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake

xi. Toilet paper zakutosha 05 ( kwa muhula mmoja )

xii. Vyombo vya chakula (**sahani ya bati yenye partition ( zinapatikana shuleni kwa Sh. 6,000/= italipiwa shuleni), bakuli, kijiko na kikombe aje navyo**);

xiii. Ndoo **kubwa 01 (lita 20** ) kwa matumizi ya ofisi na ndoo ndogo **01 (lita Kumi) rangi ya kijani kwa wavulana na pinki kwa wasichana** zenye mifuniko kwa matumizi ya mwanafunzi mwenyewe , Kwa wanafunzi wa kii*slamu wanatakiwa kuja na ndoo ndogo pinki* kwaajili ya matumizi ya mwanafunzi mwenyewe na ndoo kubwa 01 kwa matumizi ya ofisi.

## MFANO WA SARE ZA SHULE

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
|  |  |  |  |  |
| DARASANI | DARASANI | SHAMBA DRESS | SHAMBA DRESS | SHAMBA DRESS |

**SARE ZA SHULE**

i. **Wasichana** ni sketi 02 rangi ya lightblue (blue bahari) ndefu urefu cm 7 au nchi 1.5 kutoka kwenye kisigino cha kiatu, mshono linda box mbele na nyuma

ii. Rangi ya Hijab (juba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (*ambatisha mshono*);

iii. **Wavulana** ni suruali rangi nyeusi 02 upana inchi 18 inayogusa kisigino cha kiatu mifuko 03 mbele miwili na nyuma mmoja, Iwe na linda, mbili kila upande wa chini ( miguuni) ugeuzwejuu (turn up) na sivinginevyo.*;* ***SURUALI ZA MITUMBA na JEANS HAZIRUHUSIWI HAPA SHULENI****.*

iv. Mashati ni meupe **02** mikono mirefu wasichana na wavulana

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; **(Buti haziruhusiwi)**

vi. **Pull-neck** rangi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana Soksi jozi tatu wasichana nyeupe/wavulana nyeusi

vii. Mikanda ya kuvalia suruali iwe ya ngozi rangi nyeusi tu

viii. Sweta 02 rangi kijani nyeusi (kijani jeshi) na jaketi zito 01 rangi nyeusi isiyo na maandashi wala kofia

ix. Tai**-rangi nyeusi 02** kwa **wavulana** na ***wasichana ni*** *skafu* ***02*** **( rangi light-blue ) zinapatikana shuleni**

**NB.Sare za shule zote ziwekwe alama(label)jina la mwanafunzi kwenye pindo za mabega ya shati au sweta au Belt ya sketi /suruali**

**x.T-sheti 02** rangi ya kijivu zenye kola na nembo ya shule zinapatikana sshuleni kwa wasichana na wavulana

xi.Track-suit 01 rangi kijivu nzito isiyo na maandishi wala kofia kwaajili yakuvaa wakati wa kujisomea asubuhi na usiku.

**Sare ya Michezo**

i. **Wasichana** ni jezi 01 rangi bluu yenye mistari mieupe inayofanana na truck suit na sketi rangi ya damu ya mzee mshono solo urefu uzidi magoti futi 4 ,viatu vya michezo na soksi nyekundu (mistari mieupe ndefu jozi 02)
ii. **Wavulana** ni jezi 01 rangi bluu mistari mweupe inayofanana na tracksuit,viatu vya michezo, soksi za nyekundu (mistari mieupe ndefu jozi 02)
iii. Track-suit 01 rangi bluu yenye mistari mweupe mikononi **isiyo na maandishi wala kofia kwajili ya michezo**
iv. **Soksi rangi blue zenye mistari miupe ndefu kwaajili ya michezo**
v. **Pull-neck** rangi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana
vi. Nguo za kushindia (***shamba dress***)-**wasichana** ni Gauni 02 kitambaa kizito rangi ya dark blue mshono solo yenye kola nyeupe , Rangi ya Hijab (juba)(**shamba dress**) ni dark-blue ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama-( **isiwe na urembo** ) (ki*ambatisha mshono angalia*);na Nguo zakushindia (***shamba dress***)-**wavulana** ni suruali rangi kaki 02 upanainchi 18 inayogusakisigino cha kiatu mifuko 03 mbele miwili na nyuma mmoja

- NB : - Mwanafunzi anapokuja shuleni awe amevaa tracksuit rangi ya kijivu kama ilivyoelekezwa hapo juu.

**SIMU HAZIRUHUSIWI SHULENI,NI KOSA KUMILIKI SIMU SHULENI,MWANAFUNZI ASIJE NA SIMU ANAPO RIPOTI SHULE.**

**NB. (MWAFUNZI AKIKAMATWA NA SIMU atafukuzwa shule kwa kosa hilo hivyo mzazi au mlezi hakikisha mwanao haripoti na simu ,line, wala charger shuleni )**

**Aidha; Mawasiliano yote yatumike kupitia simu ya shule na si vinginevyo.**
**Namba: 0743569776.**
**Jina: MTWANGO SECONDARY SCHOOL**

**MASHARTI MENGINE**

- Mwanafunzi asije shuleni na nguo nyingine zaidi ya zile alizopangiwa vinginevyo atarudishwa nyumbani.
- Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mlinzi wa mwenzake kuzuia uovu unaweza kutokea katika chumba/bweni lao.Uharibifu wowote ule ukitokea /ukibainika katika chumba kimoja wapo kila wanafunzi wanaoishi katika chumba/bweni hilo wataadhibiwa wote,kwani wote watakuwa wameshiriki katika uharibifu wa mali ya umma.Mfano kuunganisha umeme, kuchoma bweni,kuiba vitu/mali za wenzake ,n.k
- Uharibifu wowote utakao sababishwa na mwanafunzi ni jukumu la mwanafunzi na mzazi /mlezi kugharimia matengenezo ya uharibifu huo.

**MAWASILIANO TOKA KWA MZAZI/MLEZI**

Maagizo yote ya fedha au mizigo vitumwe kwa njia ya posta tu au kupitia simu ya shule;

Namba **0743569776.**

**Jina MTWANGO SECONDARY SCHOOL**

**VIFAA VINGINE VINAVYOHITAJIKA SHULENI**

**Kutokana na uhaba wa vitendea kazi hapa shuleni , mwanafunzi anatakiwa kuja na ;-**

1.CBG – Shoka 01 na mpini wake na slasher 01,drier (squeezer 01),Toilet brush 01,chelewa 01

2.HGL - Jembe 01(lililonolewa)lenye mpini, leki,Hardbloom,Softbroom 01,chelewa 01

3.HGK – Jembe 01 na mpini wake ,slasher 01,softbloom 01,Toilet brush,chelewa 01

4. HGFa – Shoka 01 na mpini wake, Panga, drier (squeezer), soft bloom 01, toilet brush

5. HGLi - Shoka 01 na mpini wake, Panga, drier (squeezer), soft bloom 01, chelewa 03

6. HKL - Jembe 01 (lilinolewa) na mpini wake,Panga 01 (skymark machete 204-16 lililonolewa) gumu na imara, hardbloom 01, drier 01(squezeer)chelewa 01

NB. **Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na sabuni ya maji lita tano aina ya dexi kwa ajili ya usafi wa mazingira.**

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Nimarufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutoka nje ya shule bila kibali na mwanafunzi atakaye kamatwa atafukuzwa shule au **atalazimika kulipa tofari za cement (blocks 100) ili kuweka uzio imara wa shule.**

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi/Walimu anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwaruhusa na kibali maalum toka kwa MkuuwaShule. (Msiba wa mzazi au mlezi tu au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayo sababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shuleni Pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwazaidiyasiku 90 bilataarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa smwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywajiwa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara; kuvuta bangi ,kukutwa na madawa ya kulevya
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria zanchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;maeneo ya kucheza kamali
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi ,line,charger ya simu ,flash,katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba , fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi nandugu wa karibu watakaofika kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**N.B**

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza**


**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**



**Jina la Mkuu wa Shule VERONICA THOMAS MFUGALE**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**



**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0763518938**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0622730576**
- **MwandamiziTaaluma 0769444340/0754577766**
- **Mwandamizi Malezi 0752993309/0762071459**
- Namba ya Shule **0743569776.**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

**SHULE YA SEKONDARI MTWANGO,**

**S.L.P 370,**

**NJOMBE.**

**FORM NO. 1**

**MAELEKEZO BINAFSI**

1. jina lako …………………………………………………….kidato cha …………………….

Tarehe ya kuzaliwa ………………………………… namba ya cheti cha kuzaliwa ……………………………..

Mahali ulipozaliwa (wilaya) …………………………mkoani ……………………………….

Dini yako ……………………….. dhehebu …………………………..

Shule unayotoka …………………………………………………

**2. BABA**

i. Jina la Baba ………………………………………………………….

ii. Yu hai/Amefariki ………………………………………………

iii. Anuani yake kama yu hai ………………………………………………………….

iv. Kazi yake ……………………………………………………………..

v. Ameajiriwa na idara ……………………………………………………………….

vi. Dini ya Baba …………………………………….

v. Simu ya mkononi ……………………………………….

**3.MAMA** Jina la mama ……………………………………………………………….

Yu hai……………………………………………………………………

Amefariki…………………………………………………………………

Anuani yake mama kama yu hai………………………………………………

Anuani yake kama yu hai………………………………………………………

Kazi

Yake………………………………………………………………………………………

Ameajiriwa na

Idara…………………………………………………………………………………………

Dini y a

Mama…………………………………………………………………………………………

Simu ya mkononi…………………………………………………

**4. MLEZI**

i. Unaye mlezi(mlezi si mzazi lakini anakutunza na kukulipia gharama zote za mahitaji mbalimbali)

Ndiyo/Hapana……………………………………………………………

ii. Kama jibu ni ndiyo

a) Jina la mlezi: …………………………………………………….
b) Uhusiano na mlezi (mjomba,kaka,rafiki, shangazi nk)
iii. Anuani ya mlezi :……………………………………..
iv. Dini ya mlezi ……………………………………………
v. kazi yake ……………………………………………..
vi.Ameajiliwa na idara ……………………………………….
vii. Simu ya mkononi ……………………………………………..

**5. NAMBA ZA SIMU ZA NDUGU WENGINE WA KARIBU**

I. Namba …………………………………….. uhusiano ……………………………………

ii. Namba ………………………………………. Uhusiano ……………………………..

**SHULE YA SEKONDARI MTWANGO**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

A: MWANAFUNZI:JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………………….

ANUNAI: ……………………………………………………………………………………………………………………………

TAREHE: …………………………………………………………..

Mimi: ……………………………………………………………………………Nimekubali/sijakubali kujiunga na jamii ya Shule ya Sekondari Mtwango.Nimesoma maagizo ya Shule kwa makini na kuyaelewa.Naahidi kuwa mtii na nitazingatia sheria/taratibu za Shule kama nitakavyoelekezwa.

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………………….. Tarahe

B.MZAZI/MLEZI

Mimi ………………………………………………………………… Mzazi/Mlezi wa ………………………………………….

Nimesoma kwa makini maagizo ya Shule yaliyotolewa yanayohusu motto wangu.

Nimekubali /Sijakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahiddi pia kuwa nitashirikiiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia .

Sahihi ya mzazi/mlezi …………………………………………….. Tarehe……………………………………..

* Futa isiyohusika*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MKOA WA NJOMBE**

**FOMU NAMBA02**

**OFISI YA MKUU WA WILAYA,**
**WILAYA YA ……………………………,**
**S.L.P ……………………………,**
**TAREHE ……………………….**

**MKUU WA SHULE,**
**SHULE YA SEKONDARI ………………………………………**
**S.L.P ………………………**

**YAH: UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA**

Nathibitisha kuwa ………………………………………………………………..(jina kamili la mwanafunzi)

Ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kuandikishwa.
Baba yake (jina kamili)……………………………………………………….
Amezaliwa katika Mkoa wa ……………………………………… Wilaya ya ………………………………………..
Tarafa ya ……………………………………… kata ya ……………………………………
Mama yake (jina kamili) ………………………………………………..
Amezaliwa katika Mkoa wa ……………………………………… Wilaya ya ………………………………………..
Tarafa ya ……………………………………… kata ya ……………………………………

**…………………………………………….**
**MKUU WA WILAYA**

Nb. Kila mwanafunzi analazima kushughulika hati hii kikamilifu, ikisha jazwa irudishwe kwa mkuu wa shule siku ya kuriport shuleni kama una cheti cha kuzaliwa hauhitaji kujaza form hii.

**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

**FORM NO. 03**

**To be complited by medical officer in respect form V pupil's full**

Name ………………………………………………………… age ………………………….years ……………………………….

Sex……………………………………………………………………………………………………………………………

Blood count (redand white) ……………………………………………………………………………………………

Stool examination ………………………… Urine analysis

T.B Test …………………………………………………………………………………………………………………..

Ears …………………………………………………………………………………………………………………………..

Chest ………………………………………………………………………………………………………………………..

Spleen ……………………………………………………………………………………………………………………..

Abdomen …………………………………………………………………………………………………………………..

Sight ………………………………………………………………………………………………………………………….

ADDIONAL INFORMATION Physical defect or impairments infections chronic or family diseases

………………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit/unfit for admission into day/boarding school

Signature ……………………………………………………….

Designation …………………………………………………….

Station ………………………………………………………….

Date ……………………………………………….